JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU,SAYANSI NA TEKNOLOJIA

P.O Box 350 Sumbawanga, Tel: 025-280-2142, Fax: 025-280-2142 , Email: sumbawangatc@gmail.com

Unapojibu taja SBA/CCU/JI/153/19 Tarehe: 2.7.2020

Ndugu .....
.....
.....

MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA STASHAHADA YA UALIMU ELIMUYA MSINGI NA AWALI MWAKA WA MASOMO 2020/2021.

UTANGULIZI

Nafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na mafunzo ya ualimu ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi/Awali katika CHUO CHA UALIMU SUMBAWANGA kilichopo Mkoani Rukwa katika Manispaa ya Sumbawanga.

Pamoja na barua hii na kutumia maelekezo ya kujiunga na Chuo (Joining Instructions) pamoja na fomu ya uthibitisho wa afya yako kuwa inakuruhusu kujiunga namafunzo ya Ualimu (Ijazwe kabla ya kufikachuoni). Baada ya kusoma maagizo na kuyaelewa vizuri, kama unakubali kujiunga na mafunzo hayo katika Chuo hiki jiandae haraka kwa kuzingatia maelekezo yote yaliyotolewa ili uripot chuoni tarehe iliyotajwa

A: TAREHE YA KURIPOTI CHUONI.

Tarehe ya kuripotini **01/10/2019**,unapaswa kufika Chuoni siku iliyotajwa. Ukifika chuoni muone **Msajili** wa wanachuo ambaye atakupokea na kukupa maelekezo zaidi. Mwisho wa kuripoti ni tarehe **14/10/2020** endapo utachelewa kuripoti hutopokelewa na nafasi yako atapewa mtu mwingine.

B: GHARAMA YA MAFUNZO

Karo/ Ada ni Tsh**450,000**/= kwa mwaka, karo inaweza kulipwa mara moja au mara mbili tu yaani Tsh **225,000** kwa kila muhula.
Karo italipwa kupitia **mfumo wa Kielekroniki wa malipo ya Serikali (GEPG**) ambapo mwanachuo atatakiwa kuchukua namba maalumu ya kulipia **(Control number)** kwa mhasibu wa Chuo ili uweze kulipa ada ya Chuo.

C: SARE YA CHUO:

Utatakiwakuwanasare za Chuo (sutinyeusi) kama ifuatavyo:

(a)WASICHANA

Sketi ndefu juu kidogo ya kisigino nyeusi yenye rinda box nyuma (Kitambaa kizito) na blauzi ya mikono mirefu rangi ya light blue (Aina ya Kangaroo bluu bahari) .Koti jeusi lisilo na mpasuo nyuma**,** tai nyeusi**.Kwa Waislamu wataruhusiwa kuvaa hijabu nyeusi ambayo haina urembo wowote.**,Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na kisigino kirefu ,soksi nyeupe,





Mbele Nyuma

(b) WAVULANA

Suruali (Kitambaa kizito) rangi nyeusi, shati la mikono mirefu rangi ya light blue (aina ya kangaroo blue bahari).

i. Viatu vya ngozi rangi nyeusi
ii. Koti rang inyeusi aina ya suti (kujikinga na baridi)
iii. Soksi rangi nyeupe na tai nyeusi
iv. T- shirt yenye nembo ya Chuo Tsh 15,000/= Inapatikana Chuoni

NB

- ***Usishonenguo ya Kubana***, kwa wanaume surua li iwena upana wa size ya 20' katika miguu endapo utashona nguo ya kubana utalazimika kushona nyingine.Na pia koti la suti lisiwe mtumba au lisiwe na mpasuo kwa nyuma.
- ***Ili kuleta usawa wa rangi ya suti, na mashono yanayo fanana,unashauriwa ujeushonee sare kwa fundi aliye jirani na Chuo kwa gharama isiyopungua TSh 50,000 tu.***

D: MAHITAJI MENGINE YA LAZIMA

Unatakiwa kuja na michango ifuatayo:

i) Huduma ya kwanza Tsh 10,000/= kwa mawaka
ii) Ukarabati Tsh 25,000
iii) Usajili na Kitambulisho Tsh 20,000/= inalipwa mara moja mwaka wa kwanza
iv) Serikali ya wanachuo Tsh 5,000/= kwa mwaka
v) Kukodi godoro Sh 10,000/= kwa mwaka
vi) Michezosh 30,000/= kwa mwaka.
vii) Ulinzi Tsh 30,000/= kwa mwaka
viii) Usafi, mazingira na EK Sh 20,000/= kwa mwaka.

JUMLA TSH ……TSH 150,000/=

Fedha zotezilizotajwa ambayo Jumla ni Tsh **150,000/=** zilipwe akaunti ya Chuo ambayo ni **Chuo Cha Ualimu Sumbawanga** Benki ya **CRDB** akaunti namba **01J1068657500.** Fedha hizo zinaweza kulipwa kwa awamu moja au mbili kwa mwaka

ix) *Uje na Fedha sh**50,400/=** kwa ajili ya kukata bima ya afya (Kwa wale ambao hawana bima ya afya) ambapo Serikali imeagiza wanachuo wote wawe na bima ya afya, Hata hivyo kabla ya kulipa benki unatakiwa uende ofisi ya bima ya Afya ya mkoa wa Rukwa na kupewa namba maalum kwa ajili ya kwenda kulipia kielektroniki**.***

Tafadhali Fedha ya adaisiingizwe katika akaunti ya michango

E: MAHITAJI MUHIMU

Kumbuka wanachuo wote watakaa bweni na chakula kitatolewa chuoni hivyo Uje na vifaa vifuatavyo:

1. Vyombo vya Chakula na Matumizi mengine mfano Sahani, Bakuli (vyote vya udongo) na kijiko.
2. Blanketi la kujifunika (kunabaridi),shuka 2 rangi ya pink na foronya zake za kulalia pamoja na shuka moja nyeupe kwa ajili ya kufunika kitanda (Bedcover) isiwe na maua na iwe ya dukani, Chandarua
3. Nguo za Michezo (tracksuit) wakati wa michezo kila mwanachuo anatakiwa kuwa katika nguo za michezo(rangi ya light blue).

F: VIFAA VYA MASOMO

Unapaswakujanavifaavifuatavyo:

i) Madaftari ya kutosha (Counter books) kuanzia 14
ii) Karatasi ream 1 kila mwaka iwe A4
iii) Kalamu za wino za kutosha
iv) Fedha kwa ajili ya mahitajimadogomadogo (Kwa Matumizi binafsi,usafi na kununuliavifaa vya kutengenezeazana za kufundishia

***G*:SHERIA NA TARATIBU ZA CHUO.**

Mwanachuo mara afikapo Chuoni atapashwa kufuata na kuzingatia taratibu na sheria za Chuo. Hivyo mwanachuo atajaza fomu maalumu kukubaliana na sheria hizo.

H: VYETI NA VITAMBULISHO

Utasajiliwa kama utakuwa na vitu **vyote vilivyotajwa** pamoja na nyaraka zifuatazo:

i) Vyeti vya kumaliza kidato cha **NNE au SITA**(Original)chenye picha yako na mhuri wa shule yako yaani **leaving certificate**.
ii) Vyeti vya **BARAZA LA MITIHANI** vya kidato cha **NNE au SITA** (**Original Academic Certificate)** Usijena photocopy**.**

iii) Barua ya kuitwa Chuoni (Joining instructions)
iv) Fomu iliyojazwa kuthibitisha afya yako kuruhusu kuendelea na mafunzo(Ijazwe katika hospitali ya Serikali).
v) Cheti cha kuzaliwa

NB: **Hakikisha umekuja na Vyeti Original usije na copy hautaweza kusajiliwa**

HALI YA CHAKULA

Chuo hutoa Chakula kizuri kwa wanachuo wake, Chuo hakina Uwezo wa kugharamia au kutoa chakula maalum (Special diet) kwa wanachuo wenye matatizo.

J: USAFIRI

Baada ya kupata barua hii fanya mipango ya usafiri kuja Chuoni, Itakulazimu kujigharamia mwenyewe. Chuo kipo katika **Manispaa ya Sumbawanga Km 2** toka kituo kikuu cha Mabasi.

i) Wanachuo wanaotoka njia ya Mbeya kuna mabasi kama **Networking transkim, Majinjah special, Saibaba express, Mbeya Express, Newforce, Mawenink**.Unaweza kutelemkia kituo cha Chanji au Stendi Kuu
ii) Wanachuo wanaotoka njia ya Mpanda wapande mabasi ya **Amazon, Gitu, Networking transkim, Ruchoro,**wakishafika kituo kikuu cha mabasi Sumbawanga waelekee kusini mwamjiwa Sumbawanga ndipo Chuo kilipo.

Karibu sana Chuo cha Ualimu Sumbawanga.

SHAMILA I. MAKAU
MKUU WA CHUO

GOVERNMENT OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

To Medical Officer

……
……..

From ……..

……

PART A

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time teachers course.

A: 1 a) Eye-sight
b) Hearing
c) Speech
d) Venereal diseases
e) Leprosy
f) Limbs
g) Epilepsy
2. Neuroses
3. Other serious diseases

B: Blood Group

Date ……

Signature ……
Official stamp ……

PART BMEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by Government medical officer)

I have examined the above named student that he/she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for pursuing full time teacher education course.

I.a) Eye- Sight ……
b) Hearing ……
c) Limbs ……..
d) Speech ……..
e) Leprosy ……..

II Neuroses ……
III Other serious diseases ……
IV Pregnancy ……..

Date ……

Signature ……
Official stamp ……

CHUO CHA UALIMU SUMBAWANGA
KANUNI NA MWENENDO BORA WA WANACHUO

UALIMU BORA huanzachuoni, hivyo kila mwanachuo anatakiwa kuwa na mwenendo mzuri unaolinda hadhi na heshima ya kazi ya **UALIMU**. Hivyo tabia ya mwalimu inatakiwa iwe mfano mzuri kwa wanafunzi wake na kwa jumuiya nzima. Hivyo uwapo Chuoni unatakiwa kufuata kanuni zifuatazo:

1. Kujiheshimu binafsi na kuwaheshimu wengine
2. Lazima kufuata ratiba ya chuo.
3. Lazima kuvaa mavazi ya heshima na wakati wote na endapo unatakiwa kwenda nje ya Chuo itakulazimu uombe ruhusa na kuvaa Sare ya chuo.
4. Lazima uwe mlinzi wa mali za chuo (Umma) na mali yako binafsi, ukibainika kwamba ni mwizi, utasimamishwa na kuachishwa mafunzo
5. Ni marufuku Kutoro kakwenda nje ya Chuo, ikibainika hatua kali za kisheria zitachukuliwa, ikiwa ni pamoja na kuachishwa mafunzo.
6. Ni marufuku **kubeba mimba ukiwa kwenye mafunzo**, **kunywa pombe, uvutaji sigara, Uasherati, kushiriki au kutumia madawa ya kulevya, kuzurura hovyo kwenye majumba ya kupangisha (Guest house au Lodge**). Adhabu yake ni kuachishwa mafunzo.
7. Huruhusiwi kutembelea nyumba za wakufunzi au wafanyakazi isipokuwa kwakibali maalum toka ofisi ya Uadili.
8. Ni marufuku kwa wanachuo wa kiume kutembelea au kuingia mabwezi wa wasichana na pia ni marufuku kwa wanachuo wa kike kutembelea au kuingia katika mabweni ya wanaume. Adhabu yake ni kuachishwa mafunzo.
9. Mwanachuo haruhusiwi kutembelewa na wageni isipokuwasiku ya Jumapil ikuanzia saa nne (4.00) asubuhi hadi saa 8.00 mchana. Iwapo mgeni anayo shida ya haraka atamuona mkufunzi wa zamu, mwadili wa wanachuo, Makamu mkuu wa chuo au Mkuu wa Chuo kama shida yake itakuwa ni nzito sana.
10. Kutii maelekezo halali ya wakufunzi au viongozi wa serikali ya wanachuo
11. Ni marufuku kufanya mikutano yoyote bila idhini ya Uongozi wa chuo
12. Kutii kengele kila inapogongwa maanake ngelendo njia ya Mawasiliano
13. Ni lazima uonyeshe Uwezo kitaaluma kwa kuhudhuria vipindi vyote ulivyopangiwa, kufanya majaribio na mitihani yote

NB: Mara ufikapo Chuoni utapewa ufafanuzi zaidi juu ya kanuni na Mwenendo bora wa wanachuo.